

Na Rais Henry B. Eyring

Mshauri wa Kwanza katika Urais wa Kwanza



# Daima Mmkumbuke Yeye

**J**e, waweza kuvuta taswira pamoja nami nabii Moroni akiandika maneno ya mwisho ya Kitabu cha Mormoni kwenye mabamba ya dhahabu? Alikuwa peke yake.

Alikuwa ameshuhudia nchi yake, watu wake, na familia yake ikiangamia. Nchi ilikuwa “daima ni mviringo” wa vita (Moroni 8:8). Lakini bado alikuwa na matumaini, kwani alikuwa ameona siku zetu! Na katika vitu vyote ambavyo angeweza kuandika juu yake, alitualika *tukumbuke* (ona Moroni 10:3).

Raisi Spencer W. Kimball (1895–1985), alipenda kufundisha ya kwamba neno ambalo lilikuwa muhimu zaidi katika kamusi lingeweza kuwa ni *kumbuka*. Kwa sababu tumefanya maagano na Mungu, alisema, “mahitaji yetu muhimu zaidi ni kuyakumbuka”<sup>1</sup>.

Unaweza kulipata neno *kumbuka* kote katika maandiko. Wakati ambapo Nefi aliwaonya ndugu zake, mara nyingi aliwaalika wakumbuke maneno ya Bwana na wakumbuke jinsi ambavyo Mungu alikuwa amewaokoa babu zao (ona 1 Nefi 15:11, 25; 17:40).

Katika hotuba yake kuu ya buriani, Mfalme Benyaminii alitumia neno *kumbuka* mara saba. Alitumai ya kwamba watu wake wangekumbuka “ukuu wa Mungu . . . na wema wake na subira yake” kwao (Mosia 4:11; ona pia 2:41; 4:28, 30; 5:11–12).

Wakati Mwokozi alipoanzisha sakramenti, Aliwaalika wanafunzi Wake wapokee zile ishara “kwa ukumbusho” wa dhabihu Yake (Luka 22:19). Katika kila sala ya sakramenti ambayo mimi na wewe husikiliza, neno *daima linatangulia* neno *kumbuka* (ona M&M 20:77, 79).

Ujumbe wangu ni mwaliko, hata ombi, la kukumbuka. Haya ni mapendekezo matatu kuhusu kile ambacho unaweza kukumbuka kila wiki wakati unapopokea ishara

takatifu za sakramenti. Ninatumaini yatakusaidia kama yalivyokuwa kwangu.

## Mkumbuke Yesu Kristo

Kwanza, mkumbuke Mwokozi. Kumbuka alikuwa nani alipokuwa duniani, jinsi alivyozungumza na wengine, na jinsi alivyoonyesha ukarimu katika matendo Yake. Kumbuka alishinda na kina nani na yale aliyofundisha. Mwokozi “akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema” (Matendo ya Mitume 10:38). Aliwatembelea wagonjwa. Alikuwa amejitolea kutimiza mapenzi ya Baba Yake.

Zaidi ya yote, tunaweza kukumbuka gharama kubwa ambayo Alilipa, kutokana na upendo Wake kwetu, kutoa doa la dhambi zetu. Tunapomkumbuka, nia yetu kumfata itakua. Tutataka kuwa wakarimu zaidi kidogo, wenye kusamehe zaidi, na wenye kutaka sana kutafuta kujua mapenzi ya Mungu na kuyatimiza.

## Kumbuka Kile Unachohitaji Kukifanya Vyema Zaidi

Ni vigumu kufikiria kuhusu Mwokozi—Usafi na Ukamilifu Wake—bila ya kufikiria pia kuhusu jinsi tulivyo na dosari na tusio wakamilifu tukijilinganisha Naye. Tumefanya maagano kushika amri Zake, lakini mara nyingi tunashindwa kufikia kiwango hiki cha juu. Lakini Mwokozi aliju hili lingetokea, ndio maana alitupa ibada ya sakramenti.

Sakramenti ina mizizi katika agizo la Agano la Kale la kutoa dhabihu, ambalo lilijumuisha ungamo la dhambi (ona Mambo ya Walawi 5:5). Hatutoi dhabihu ya wanyama tena, lakini bado tunaweza kuacha dhambi zetu. Maandiko huita dhabihu hii ya “moyo uliyopondeka na roho iliyo-vunjika” (3 Nefi 9:20). Njoo kwenye sakramenti na moyo

wenye kutubu (ona M&M 59:12; Moroni 6:2). Unapofanya hivyo, utapokea msamaha wa dhambi na hautapotea kuto-ka kwenye njia inayokurejesha kwa Mungu.

### Kumbuka Maendeleo Unayofanya

Unapochunguza maisha yako wakati wa ibada ya sakramenti, ninatumai ya kwamba mawazo yako hayatalenga tu kwenye vitu ambavyo hukufanya vyema lakini pia kwenye vitu ambavyo umeweza kufanya vyema—nyakati amba-zo umeweza kuhisi ya kwamba Baba wa Mbinguni na Mwokozi walikuwa wamefurahishwa nawe. Wawea hata kuchukua nafasi wakati wa sakramenti kumuuliza Mungu akusaidie uone mambo haya. Ikiwa utafanya hivyo, ninauhidi utahisi kitu fulani. Utahisi matumaini.

Wakati nimefanya hivi, Roho amenithibitishia ya kwa-omba wakati bado niko mbali na ukamilifu, hali yangu ya leo ni bora kuliko ilivyokuwa jana. Na hili linanipa ujasiri kwamba, kwa sababu ya Mwokozi, ninaweza hata kuwa bora zaidi kesho.

*Daima* ni muda mrefu, na humaanisha juhudini zenyefokasi nydingi. Unafahamu kutokana na uzoefu jinsi ilivyo vigumu kufikiria moyoni kuhusu jambo moja kila wakati. Lakini bila kujali ni vizuri kiasi gani unavyoweka ahadi yako ya daima kumkumbuka, Yeye hukukumbuka daima.

Mwokozi anafahamu changamoto zako. Anafahamu jinsi gani ilivyo kuwa na shida za maisha zikiwa zinakule-me. Anajua jinsi unavyohitaji kwa haraka baraka ambayo hutokana na kumkumbuka daima na kumtii Yeye—“ili [wewe] uweze *daima* kupata Roho wake kuwa pamoja [nawe]” (M&M 20:77; imetiliwa mkazo).

Basi, Anakukaribisha tena kwenye meza ya sakrameni kila wiki, kwa Mara nyingine akikupa nafasi ya kutoa ushuhuda mbele Yake kwamba daima utamkumbuka.

### MUHTASARI

1. Spencer W. Kimball, “Circles of Exaltation” (hotuba kwa waalimu wa kidini wa Mfumo wa Elimu wa Kanisa, Juni 28, 1968), 5.

### KUFUNDISHA KUTOKA KWENYE UJUMBE HUU

Maisha yanaweza kuwa yenyeye msisimko na shughuli nydingi na kusababisha iwe vigumu kwetu kumkumbuka Mwokozi wetu Yesu Kristo daima. Sakramenti, hata hivyo, inatoa nafasi maalum kila wiki tunapoweza kutafakari kuhusu maisha na mafundisho Yake. Pamoja na wale unaowafundisha nyumbani, zingatia jinsi unavyotumia nyakati hizo tulivu sasa, na jadili jinsi unavyoweza kufokasi zaidi kwa Mwokozi. Unawezaje kutumia nyakati hizi ili kutafakari juu ya yale unayoweza

kuboresha wewe binafsi? Nini thamani ya kukumbuka maendeleo unayofanya kila wiki?

## VIJANA

### Mambo Matatu ya Kukumbuka

**N**eno kumbuka linaonekana mara nyingi katika Kitabu cha Mormoni. Nefi aliwahimiza ndugu zake kukumbuka jinsi Mungu alivyowaokoa mababu zao. Mfalme Benyamini aliwaomba watu wake wakumbuke ukuu wa Mungu. Na Moroni aliwaagiza wasomaji wake wakumbuke jinsi Bwana amekuwa na huruma.

Kumkumbuka Mwokozi ni muhimu—hata tunaaga-na kumkumbuka kila wakati tunapopokea sakramenti. Rais Eyring anaturalika tukumbuke mambo haya matatu wakati wa sakramenti.

1. **Mkumbuke Yesu Kristo:** Soma maandiko kuhusu jinsi Mwokozi alivyohudumu na kuonyesha upendo kwa wengine. Unahisi vipi kuhusu upendo Wake? Ni namna gani unaweza kuhudumu na kuonyesha upendo kwa wengine jinsi Mwokozi alivyofanya?
2. **Kumbuka kile unachohitaji kuboresha:** Tafakari kuhusu wiki yako iliyopita kwa moyo wenye kutaka kutubu. Chagua kitu kimoja ambacho unaweza kubadili, na uandike jinsi utakavyofanya maboresho hayo. Weka lengo lako mahali ambapo utaweza kuliona kila mara.
3. **Kumbuka maendeleo unayoyafanya:** Muombe Mungu akuonyeshe maendeleo mazuri unayofanya. Weka kumbukumbu ya jinsi unavyohisi.

Sisi sio wakamilifu, lakini Mwokozi anafahamu hivyo. Ndio maana anatuomba tumkumbuke. Kumkumbuka kunatupatia matumaini na hutusaidia kutaka kufanya vizuri zaidi. Hata wakati ambapo tunashindwa kumkumbuka, Rais Eyring anasema, “Daima anakukumbuka.”

“Mngekumbuka jinsi vile Bwana amekuwa na huruma” (Moroni 10:3).

## WATOTO

### Kumkumbuka Yesu

**M**aandiko yanafundisha kwamba tunapaswa daima kumkumbuka Yesu Kristo. Hii humaanisha kwa-omba tunapaswa kufikiria sana kumhusu Yeye sana na kufuata mfano Wake.

Weka picha ya Yesu mahali ambapo utaweza kuiona kila mara.

“Na ikiwa mnanikumbuka daima Roho yangu ituku-wa nanyi” (3 Nefi 18:7).



# Pata Kumjua Yeye na Familia Yake

*Ualimu wa kutembelea unahusu kupata kumjua kila dada na kumpenda kila dada ili tuweze kumsaidia kuimarisha imani yake na kutoa huduma.*

**Imani, Familia, Usaidizi**

Rita Jeppeson na mwalimu wake mtembeleaji wamekuwa marafiki wazuri wakati ambapo walikuwa wakitembeleana na kushiriki kanuni za injili. Lakini kutembeleana kwao pia ni pamoja na kucheza michezo ya kuunda maneno pamoja. Ni kitu kinachompendeza Rita zaidi kuhusu mwalimu wake mtembeleaji kwa sababu anafahamu ya kwamba wao ni marafiki na matembezi hayo sio tu jambo la “kutia alama kuonyesha kukamilika” kwenye orodha. Kuna mambo mengi ambayo kina dada wanaweza kufanya wakati wa matembezi, kama vile kutembea pamoja au kungo'a magugu katika bustani huku watoto wakicheza.

Mzee Jeffrey R. Holland wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili alisema, “Jitazameni kama wajumbe wa Bwana kwa watoto Wake. . . Tunetumaini . . . kwamba mtaanzisha, kipindi cha uhalisia, cha kiinjili juu ya kuwajali waumini, kuwaangalia

waumini na kujaliana, mkishughulikia shida za kiroho na kimwili kwa njia yoyote inayoleta usaidizi.”<sup>1</sup>

Bwana kuititia Musa aliwaamuru wana wa Israeli kwamba “Mgeni akaaye pamoja nawe atakuwa kama mzaliwa kwenu, mpende kama nafsi yako (Mambo ya Walawi 19:34). Kina dada ambao tunawatembelea na kuwafundisha wanaweza kuwa “wageni” tunapoanza huduma yetu, lakini tunapopata kumjua pamoja na familia yake, hamu yetu itaongezeka “kubeba mizigo ya mmoja na ya mwingine, ili iwe miepesi” na kuwa “mioyo yetu iunganishwe pamoja kwa umoja na kwa upendo mmoja kwa mwingine” (Mosia 18:8, 21).

Reyna I. Aburto, Mshauri wa Pili katika Urais Mkuu wa Muungano wa Usaidizi wa Kina Mama, hukumbuka wakati aliquwa muumini mpya wa kanisa aliyetalikiwa karibuni. “Waalimu wangu wa kutembelea walikuja nyumbani kwangu,”

alisema, “na walileta hisia njema za kujumuishwa na upendo katika moyo wangu.”<sup>2</sup>

## Zingatia Hili

Katika familia za kina dada ambao wewe unawatembelea kuwafundisha, ni matukio gani muhimu yajayo ambayo unapaswa kuyajua na kuyakumbuka?

### MUHTASARI

- Jeffrey R. Holland, “Wajumbe wa Kanisa,” *Liahona*, Nov. 2016, 62.
- Reyna I. Aburto, “Muungano wa Usaidizi wa Kina Mama Umekuwa Nini Kwangu?” Mkutano Mkuu wa Wanawake kule Brigham Young University, Mei 5, 2017, LDS.org.

### Uhudumiaji

Tunapomfahamu vyema na kumpenda kila dada tunayemtembelea na kumfundisha pamoja na familia yake, tutapokea msukumo wa kibinasi ili tupate kujua jinsi ya kushughulikia mahitaji ya kiroho na ya kimwili ya kila mmoja.